

FAHAMU KUHUSU DIRA ZA MAJI ZA DAWASCO

Dira/Mita ni kifaa kinachotumika kufanya uhakiki wa kujua kiwango halisi cha matumizi ya Maji yaliyotumiwa na mteja. Ni lazima mteja afungiwe Mita ya Maji ili kupata rekodi sahihi ya matumizi yake ya Maji kwa muda wa mwezi badala yakupata ankara za makadirio.

Dira za Maji zipo ambazo zinatumia umeme (Electro Magnetic) na ambazo hazitumii umeme (Non Electro Magnetic) ambazo zinasoma kutokana na msukumo wa Maji.

Dira ambazo hutumiwa na Dawasco.

- ✓ **Sensus**
- ✓ **Kent**
- ✓ **Baylan**
- ✓ **Kmei**
- ✓ **Abfar**
- ✓ **Gkmj**
- ✓ **Fuju**
- ✓ **Siemens**
- ✓ **Ge panametrics**

DAWASCO ndio wenye jukumu kuu la kuhakikisha kuwa kila mteja wake anafungiwa dira ya Maji, hata kama mteja atakuwa si mmiliki wa nyumba ni mpangaji pia ana haki ya kufungiwa dira ya Maji kwenye nyumba anayoishi ilimradi awe amelewana na mwenye nyumba.

Hivyo wateja wote ambao wana akaunti namba lakini bado hawajafungiwa dira za maji wahakikishe wanafika kwenye Ofisi za DAWASCO ili kupata huduma hiyo. Ili kufungiwa mita ya Maji, mteja atalazimika kulipia kiasi kidogo cha fedha kilichopangwa kwa ajili ya gharama ya mita na vifaa vingine vidogovidogo, mteja hatahitajika kulipia gharama zingine zozote zikiwamo za mafundi.



Mfano wa Dira anayofungiwa mteja wa kawaida ambayo haitumii umeme kuonyesha kiwango cha matumizi ya Maji

Anayehusika katika usomaji wa dira

DAWASCO ndio wenye jukumu la kuhakikisha kuwa dira zote za Maji zinasomwa kila mwezi, na mteja analipia bili yake kutokana na kiasi cha Maji alichotumia ndani ya mwezi huo. Endapo dira yake haitasomwa kwa wakati mteja anaweza kutumiwa bili ya makadirio. Ili kuepuka kulipia bili ambayo imefanyiwa makadirio mteja pia ana nafasi ya kusoma dira yake na kuzifikisha katika Ofisi za DAWASCO zilizopo karibu yake muda wowote. Ni jambo zuri pia kwa mteja kujijengea mazoea ya kusoma uniti zake za Maji nakuelewa matumizi yake ya Maji na pia itamsaidia kujua kiurahisi zaidi tofauti zitakazojitokeza kwenye bili yake. Na endapo kutakuwa na tatizo kwenye dira yake atagundua kirahisi na mapema zaidi.

Umasoji wa Dira ya Maji

Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kumfanya mteja kujenga mazoea ya kujisomea dira yake ya Maji, ikiwamo ya kutaka kujua ni kiasi gani cha Maji anakitumia nyumbani kwake, pia kutaka kujua kama dira yake inavujisha Maji. Hivyo anachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kuwa anafungua mfuniko wa juu wa dira yake, na kisha kusoma namba zinaonekana kwa juu kwenye dira yake, akianza upande wa kulia na kumaliza upande wa kushoto wa mita yake.

Faida za kufungiwa Dira ya Maji

Kuwa na dira ndio njia pekee na iliyo halali kwa mteja katika kulipia bili yake, wateja wengi wenye dira mara nyingi hulipia kiasi kidogo kwani hulipa kutokana na matumizi yake.

- ✓ Endapo mteja atafungiwa dira ya Maji atakuwa na nafasi kubwa ya kujua kiasi gani cha Maji kinachotumika nyumbania kwake kwa siku au mwezi, hivyo atalipa kutokana na matumizi yake.
- ✓ Ufungaji wa mita utamsaidia mteja kudhibiti kiwango cha matumizi ya Maji, kuokoa hela kwa kulipia kiasi kidogo cha bili ya Maji endapo matumizi yake ya Maji yatakuwa madogo, hivyo kiasi cha fedha atakachoweza kuokoa kitategemeana na matumizi yake ya Maji.
- ✓ Itasaidia kupunguza mivujo ya Maji (Leakages), dira itaonyesha kama kuna mvujo kwenye bomba kutokana na dira hiyo kuendelea kusoma licha ya bomba hilo kufungwa

Dira ya Maji hufungwa kwa Mteja kwa masharti yafuatayo:

- ✓ Dira zinafungwa na mafundi wa Dawasco tu, na sio mtu mwingine yeyote
- ✓ Mteja haruhusiwi kuifungua, kuitengeneza, kuihamisha sehemu ilipofungwa ikapelekea kuharibika.
- ✓ Ikiwa Mita ya Maji itaharibiwa, Mteja atapaswa kulipia gharama za kununua dira ya Maji nyingine kwa bei itakayokuwa inauzwa kwa wakati huo vinginevyo atalazimika kukosa huduma ya majisafi na salama.
- ✓ Mteja anatakiwa kutunza dira yake kuepuka uharibifu utakaoweza kujitokeza ili kuepuka usumbufu wa kuilipia tena na kusitishiwa huduma ya Maji.

Mwenye jukumu la kufanya matengenezo ya dira za Maji

Dawasco ndio wenye majukumu yote ya kufanya matengenezo ya dira zote za wateja ambazo zinaonekana kuwa na matatizo, mteja hana ruhusa ya kufungua mita ambayo anahisi inahitaji matengenezo, endapo atagundua kuwepo kwa tatizo anachotakiwa kufanya ni kutoa taarifa kwenye ofisi za Dawasco na mafundi watafika kufanya ukaguzi kubainisha tatizo. Mteja hataingia gharama yoyote kwa ajili yakufanyia matengenezo mita yake au kuibadilishia .

Hivyo ni vema kwa wateja wote DAWASCO wakahakikisha wanapata huduma ya kufungiwa dira ya Maji, pia ni jukumu la mteja kuhakikisha analinda na kuitunza dira yake, ili isiibiwe na kucheze na mtu yeyote, Lakini vilevile kama mteja ataonekana kuhusika na kuharibika au kuibiwa kwa mita hiyo atalazimika kuilipia.